

Ijue Machi 8

Siku ya wanawake duniani huadhimishwa ifikapo machi 8 ya kila mwaka ambapo hulenga zaidi kutoa hamasa kwa wanawake na kutathmini maendeleo yao hasa katika ngazi ya uchumi, siasa na hata kiutamaduni ili kuweza kuleta usawa wa kijinsia miongoni mwa jamii.

Siku hiyo kwa mara ya kwanza ilifanyika kutokana na jitihada za wanawake 15,000 mwaka 1908 walipoandamana mjini New York, Marekani wakidai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, kupatiwa ujira wa kuridhisha na haki ya kupiga kura.

Maadhimisho ya kwanza kuwa na kaulimbiu yalikuwa ni mwaka 1996 ambayo ilikuwa ni "furahia yaliyopita, panga kwa ajili ya baadae", na kwa mwaka huu yanaadhimishwa kwa kaulimbiu isemayo "kizazi cha usawa kwa maendeleo ya Tanzania ya sasa na baadae".

Kabla ya kufikia kilele cha maadhimisho hayo, wanawake kote duniani huhamasishana na kukumbusha juu ya wajibu wao katika kushiriki mambo mbalimbali yanayoweza kuwawezesha kupiga hatua kimaendeleo katika kuifikia 50-50 ya usawa wa kijinsia baina yao na wanaume.

Kutokana na takwimu mbalimbali zinaonyesha idadi ya wanawake ni wengi duniani ukilinganisha na wanaume, lakini kundi hili kubwa liko nyuma kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili ikiwemo mila kandamizi zinazowanyima uhuru na nafasi ya kushiriki katika mambo ya kimaendeleo hasa maswali ya umiliki mali na ushiriki katika kutoa maamuzi.

Mbali na changamoto hizo pia lipo kundi kubwa la wanawake ambao wamepiga hatua na ni chachu na hamasa kwa wanawake wengine, ambao wamekuwa wakiamini katika kuwa tegemezi na kusahau kujitegemea wenyewe katika kufanya kazi mbalimbali zitakazowawezesha kuondokana na hali ya utegemezi.

Nchini Tanzania wanawake wenye uthubutu na wanaoonekana kuwa wa mfano kwa wasichana wadogo wanaoendelea kukua

miongoni mwao ni Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe ambae ameonekana kuwa chachu kwa wasichana wenye ndoto kubwa kiuongozi, Joketi Mwegelo.

Wakati umefika sasa wa jamii kuutambua na kuuthmini mchango wa wanawake ambao wanafanya mambo ambayo yanawainua wao na jamii kwa ujumla, ili tuweze kujenga kizazi imara, chenye upendano na chenye uthubutu.

Wakati umefika sasa wa kupima mafanikio katika maeneo ya kipaumbele kama yalivyobainishwa katika azimio la Beijing, nchini Chini kubainisha changamoto na kutafakari kwa kina namna ya kupiga hatua kumkomboa mwanamke na kujitathmini ni kwa kiasi gani hapa Tanzania tumefanikiwa kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuwasaidia kuondokana na umasikini.

Pia kuwapatia wanawake haki na kuwaongezea uwezo kisheria, kwa wanawake wote ambao wana elimu Kuhakikisha kuwa wanapata ajira zenye staha, tuhakikishe wanawake wanashirikishwa katika maamuzi mbalimbali katika jamii yetu, hiyo yote ni katika utekelezaji wa kuwawezesha wanawake katika uongozi kuifikia asilimia 50-50 kati ya wanawake na wanaume katika nafasi zote za maamuzi kwenye ngazi zote.